

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**


Simu:+255 22 211-3139, +255 22

211 0146-10

Nukushi: +255 22 2135486

Tovuti: [www.moe.go.tz](http://www.moe.go.tz)

*Unapojojibu Tafadhali Taja:*



S.L.P. 9121,  
7 Mtaa wa Magogoni,  
11479 DAR ES SALAAM.

Kumb.Na.ED/OKE/NE/Vol.1/01/73

Tarehe: 19/9/2016

Makatibu Tawala (M)

Makatibu Tawala (W),

Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule (K),

Wathibiti Wakuu wa Ubora wa Shule (W),

Wakuu wa Shule zisizo za Serikali,

**TANZANIA BARA.**

**WARAKA WA ELIMU NA. 4 WA MWAKA 2016  
MWONGOZO WA UUNDAJI WA KAMATI ZA SHULE**

Kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na rekebisho Na. 10 la mwaka 1995 kila shule ya msingi sharti iwe na Kamati ya Shule iliyo hai.

Ufuatiliaji katika shule mbalimbali hapa nchini umebainisha kuwa Kamati nyingi za shule hazipo hai na chache zilizopo hazikidhi matakwa ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014. Hivyo basi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa maelekezo ya uundaji upya wa Kamati za Shule.

**Waraka huu unaelekeza yafuatayo:**

- i. Mionganii mwa wajumbe watakaouna Kamati ya Shule, wawepo wawakilishi wa wajumbe wa Serikali za Vijiji/Mitaa.
  - ii. Uteuzi na uchaguzi wa wajumbe wa Kamati za Shule pamoja na sifa nyingine stahiki uzingatie sifa za msingi ambazo ni uwezo wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.
  - iii. Kamati ya shule itachaguliwa na kikao cha wazazi.
  - iv. Kamati ya Shule itakuwa na wajumbe kumi na tatu (13) na itafanya kazi kwa muda wa miaka mitatu. Hata hivyo, wajumbe wa Kamati wanaweza kuchaguliwa tena kwa kipindi kingine cha miaka mitatu. Ujumbe katika Kamati utakoma baada ya kipindi cha mihula miwili ya miaka mitatu kwa kila muhula.
- v. **Wajumbe watakaouna Kamati za Shule:**
- (a) Mwenyekiti: Awe ni mkazi wa eneo hilo na pia awe na cheti cha kuhitimu Elimu ya Sekondari au zaidi.
  - (b) Makamu Mwenyekiti: Awe na sifa kama za Mwenyekiti.
  - (c) Katibu: Atakuwa ni Mwalimu Mkuu wa Shule husika.

- (d) Mwalimu wa Taaluma katika shule: Mjumbe.
- (e) Mwakilishi mmoja wa walimu atakayechaguliwa na walimu.
- (f) Afisa Elimu Kata: Mjumbe.
- (g) Wajumbe wawili (2) kutoka Serikali ya Kijiji/Mtaa kwa kuzingatia jinsi.
- (h) Wajumbe watano (5) waliochaguliwa na wazazi kutoka mionganini mwa wazazi/walezi wa wanafunzi wanaosoma katika shule hiyo.

**Tanbihi:** Waheshimiwa Wabunge, Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji/Mitaa wasiwe sehemu ya wajumbe wa Kamati za Shule.

**vi. Kamati ya Shule itakuwa na wajibu pamoja na majukumu yafuatayo:**

- (a) Kuandaa Mpango wa Maendeleo ya Shule na Mpango kazi wa Shule (Whole School Development Plan and School Action Plan).
- (b) Kubuni na kupanga mikakati ya maendeleo ya shule.
- (c) Kusimamia utekelezaji wa utoaji wa elimu bora.
- (d) Kuhimiza uwajibikaji na nidhamu katika shule.
- (e) Kuitisha vikao vya wazazi na kutoa taarifa ya maendeleo ya shule.
- (f) Kuandaa bajeti na kusimamia matumizi ya fedha za shule.
- (g) Kuidhinisha matumizi ya fedha za shule.
- (h) Kusimamia ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule.
- (i) Kuhimiza usafi, afya bora za wanafunzi na utunzaji wa mazingira.
- (j) Kusimamia matumizi bora ya fedha za uendeshaji wa shule.
- (k) Kutoa taarifa kwenye Serikali ya Kijiji/Mtaa juu ya maendeleo ya shule.
- (l) Kusimamia upatikanaji wa chakula cha mchana kwa wanafunzi.

vii. Idadi ya vikao vya kamati ya shule isipungue vinne kwa kila muhula.

**viii. Kamati ya Shule iunde Kamati ndogo ndogo zifuatazo:-**

- (a) Kamati ya Fedha na Mipango.
- (b) Kamati ya Miundombinu na mazingira.
- (c) Kamati ya Taaluma na nidhamu.
- (d) Kamati ya Afya na Chakula.
- (e) Kamati ya Malezi na Ushauri Nasaha.

Waraka huu unaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Oktoba, 2016 na unafuta Waraka wa Elimu Namba 14 wa Mwaka 2002.



Nicolas J. Buretta  
**KAIMU KAMISHNA WA ELIMU**

**Nakala:** Katibu Mkuu,  
 Ofisi ya Rais - TAMISEMI,  
 2 Barabara ya Nane,  
 S.L.P 1923,  
**DODOMA.**